

Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari

Siku 16 za Uanaharakati mwaka wa 2026

Katika mwaka wa 2026, tunaungana katika kampeni ya Siku 16 ya Uanaharakati chini ya dhamira yetu ya **“Tengeneza Upya Mamlaka Yetu: Hatua za pamoja kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake”** na kaulimbiu *“Wezesha. Chukua Hatua. Tengeneza Mustakabali wa Baadae.”*

Madhumuni ya Mwongozo Huu

Mwongozo huu umeandaliwa ili kutoa maelekezo kwa njia ya vitendo jinsi ya kuwasiliana, kupanga, kuhamasisha, na kupanua kampeni ili iweze kufikia watu wengi. Unatoa zana, mawazo, na shughuli zilizopendekezwa ili kukuza sauti ya kifeministi, kuimarisha mshikamano, na kuhamasisha hatua za pamoja za kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Pia inawahamasisha wanachama na washirika kutumia majukwaa mbalimbali ya mawasiliano na mbinu zenye ubunifu ili kushirikisha jamii, kushiriki jumbe za kampeni, na kudumisha hatua za kifeministi hata baada ya kipindi cha kampeni.

Tumia mwongozo huu kwa kunyumbulika: chagua vitendo vinavyoendana na muktadha wako, badilisha lugha kwa ajili ya jamii yako, na fanya kazi kwa pamoja na vyombo vya habari vya ndani na mitandao, na shughuli za kijamii inapowezekana. Mwongozo huu unajumuisha zana kuu nne:

a. Kampeni za mitandao ya kijamii na hashtag
b. Ushiriki wa vyombo vya habari vya ndani kupitia redio na televisheni
c. Shughuli za jamii na vikundi
d. Habari za ndani na ushiriki wa vyombo vya habari, ikijumuisha mfano wa taarifa kwa vyombo vya Habari

16 DAYS

GBV PREVENTION NETWORK

UN TRUST FUND TO END VIOLENCE AGAINST WOMEN AND GIRLS

1. Kampeni ya Mitandao ya Kijamii

Jiunge na kampeni ya kanda kwa kutumia majukwaa yako ya mitandao ya kijamii ili kukuza sauti za kifeministi, kuimarisha mshikamano, na kujenga maono ya pamoja kwa mustakabali wa kifeministi. Kama sehemu ya nakala ya mtandaoni ya kiti ya kuchukua hatua na Utetezi ya Siku 16 ya Uanaharakati, tutashirikisha vibonzo vya mitandao ya kijamii na nyenzo zingine za kampeni unazoweza kutumia na kuzibadilisha ili kushirikisha katika mitandao yako, kuchochea mazungumzo, na kuhamasisha hatua za pamoja ili kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Unapoandaa na kushirikisha maudhui, toa kipaumbele kwaajili ya kuheshimu utu, faragha, na usalama wa kila mtu anayehusika. Epuka kushirikisha maelezo ya wahanga walio tambuliwa, picha, nukuu, au hadithi zao, watoto, au wanajamii bila ridhaa yao. Tutumie majukwaa yetu ya kidijitali kwa njia ya uwajibikaji ili kukuza utamaduni wa kuheshimiana, mshikamano, na kujenga nafasi salama mtandaoni.

Fuatilia na Utag kwenye @preventgbvnet.bsky.social on Bluesky, preventgbvnet kwenye Instagram, na kwenye mtandao wa Kuzuia UWAKI kwenye Facebook.

Tumia lebo hizi za hashtag:

#16DaysOfActivism#RenewOurPower
#EmpowerActShapeTheFuture

Mambo Unayoweza Kufanya Mtandaoni

i. Shirikisha wengine jinsi kikundi au jamii yako inavyofanya kazi ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

ii. Tuma mtandaoni ujumbe wenye matumaini, kuimarisha, mshikamano, na wenye kuunga mkono.

iii. Himiza umuhimu wa kuheshimu utu, faragha, kutoa ridhaa, na usalama mtandaoni.

iv. Kamwe usishirikishe au kusambaza picha au maudhui yanayohitaji faragha bila ridhaa ya mhusika.

v. Tumia majukwaa yako kuzuia madhara ya mtandaoni na hamasisha heshima, usalama, na uwajibikaji.

vi. Tumia na shiriki kwenye lebo za hashtags za kampeni ili kusaidia kusambaza na kukuza ujumbe wa kampeni hiyo katika ngazi ya kimataifa na kikanda.

Ujumbe wa Kuimarisha

i. Anzisha mazungumzo ya jinsi kukosekana kwa ufadhili na upungufu wa rasilimali unavyoathiri vuguvugu za kifeministi, huduma muhimu, na kazi ya kuzuia ya kijamii.

ii. Shirikisha michoro rahisi, hadithi, au nukuu zinazoonyesha athari ya kupungua kwa ufadhili.

iii. Angazia mwitikio wa harakati kupitia mshikamano, kujijali kwa pamoja, ubunifu, na ustahimilivu.

iv. Fanya kazi na viongozi wa jamii, wanaharakati vijana, na watu wenye ushawishi kushirikisha jumbe za kampeni na kuhamasisha usalama wa mtandaoni.

v. Toa taarifa ya jinsi ya kukabiliana na unyanyasaji wa mtandaoni na uandae vipindi vifupi kuhusu namna ya kujilinda kidijitali.

2. Vyombo vya Habari vya Kijamii

Redio,Televisheni, ushiriki wa magazeti

Ikiwa shirika lako lina uhusiano na vituo vya redio au televisheni, tumia majukwaa hayo kukuza sauti za kifeministi, kusherehekea hatua za pamoja, na kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kuwekeza katika kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake. Shirikiana na wadau wa vyombo vya habari kuandaa vipindi vya mazungumzo, mahojiano, mijadala na makundi mbalimbali ya watu, utangazaji wa shughuli za kampeni na programu zingine zinazoangazia jitihada za kifeministi, kushirikishana uzoefu, na hamasisha kuchukua hatua.

Unapopanga shughuli za kijamii au kushirikisha vyombo vya habari, anza kwa kutumia mbinu za msingi za usalama na kujijali kwanza. Hizi zinatakiwa kuzingatia usiri, ridhaa baada ya mhusika kupata taarifa, upatikanaji wa taarifa za rufaa, na mwongozo unaoeleweka kuhusu upatikanaji wa huduma kwa mtu yeyote ambaye anaweza kuhitaji usaidizi. Hakikisha kwamba shughuli zote zinadumisha utu, faragha, na usalama wa washiriki.

Fikiria jinzi unavyoweza kutumia majukwaa haya ili:

i. Kuandaa majadiliano na wanaharakati wa kifeministi, viongozi wa jamii, na wataalamu.

ii. Kushirikisha hadithi za wahanga ikiwa umepata ridhaa yao baada ya kuwapa taarifa, hakikisha ulinzi, na mpango unaoeleweka wa kulinda faragha na utu wao.

iii. Kuchambua masuala mbalimbali kama vile ukatili wa mtandaoni, kuminywa kwa nafasi ya kiraia, na mapengo ya ufadhili unaohitajika.

iv. Kuangazia vikundi vya jamii vinavyoendeleza haki za wanawake na wasichana.

v. Kuhamasisha shughuli za Siku 16 zinazoamsha ari ya kuchukua hatua, mshikamano, na nguvu ya pamoja.

3. Shughuli za Kijamii na Vikundi

Andaa Wakati mzuri na jamii katika kipindi cha Siku 16 za Uanaharakati. Unaweza:

i. Kuandaa mazungumzo kuhusu usalama mtandaoni au kuwasaidia wahanga wa ukatili.

ii. Kuandaa harambee ya ndani ili kuimarisha kikundi chako au kusaidia shirika linalo tetea haki za wanawake.

iii. Kuchora michoro ya Ukutani au ukumbi wa sanaa yenye ujumbe wa matumaini, ustahimilivu, na mshikamano.

iv. Kuandaa kusanyiko la watu kwa ajili ya tukio la simulizi za hadithi ambapo wahanga, wazee, na wanajamii wanaweza kushiriki ili kutoa maneno ya hekima, kwaajili ya uponyaji, na kuungana kwa pamoja.

4. Fanya kazi na Vituo na Vyombo vya Habari vya Ndani

Kushirikiana na Vituo na vyombo vya habari vya ndani kunaweza kusaidia kusambaza ujumbe wako kwa upana zaidi wakati wa Siku 16 za Uanaharakati. Fikiria vidokezo hivi vya vyombo vya habari:

i. Kabla ya kuwasiliana na vyombo vya habari, andaa ujumbe muhimu, msemaji, maelezo yanayohusu tukio, mahitaji ya ridhaa yanayotakiwa, na picha au nukuu zozote ambazo zinaweza kushirikishwa kwa njia salama.

ii. Andika makala fupi au vipande vya maoni kuhusu masuala kama vile unyanyasaji wa mtandaoni au changamoto za ufadhili.

iii. Shirikisha hadithi zenye nguvu kutoka katika jamii yako zinazohusu ustahimilivu na mabadiliko.

iv. Sherehekea ushindi uliopatikana hata kama ni mdogo ili kuhamasisha na kuunganisha jamii yako.

Kwa Nini Hatua za Pamoja ni Muhimu

Dhamira ya **"Tengeneza Upya Mamlaka Yetu: Hatua za pamoja Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake"** inatambua kwamba ukatili dhidi ya wanawake umejikita katika mizizi ya kutokuwepo kwa usawa wa mamlaka, kanuni potofu zitokanazo na mila, na mifumo inayowezesha na kuendeleza ukatili. Kwa hivyo, njia Madhubuti za kuzuia zinahitaji mbinu zaidi ya kuongeza uelewa, inahitaji jamii na vuguvugu la uanaharakati kupanga, kupinga kanuni potofu zitokanazo na mila, kuimarisha uwajibikaji, kuendeleza usawa, na kubadilisha mashariti yanayoruhusu ukatili kuendelea. Zaidi ya yote, inatoa wito kwetu sote kutengeneza mustakabali wa baadae.

> **" Kutengeneza upya mamlaka yetu kunamaanisha kwamba kuzuia ukatili kwa njia ya kudumu kunahitaji kazi ya pamoja. Lazima tulinde nafasi ambazo watu wameandaa, kuwekeza katika harakati za kifeministi na kuzuia ukatili, kujijali kwa wale wanaofanya kazi ya kuzuia ukatili, na kujenga mazingira ya jamii kuongoza mabadiliko ya kudumu."**

Mtandao pia unasisitiza kujijali kwa hali ya juu ni muhimu ili kuendeleza harakati. Kujijali kuna mapana zaidi ya kujijali binafsi ili kujumuisha tabia ya pamoja ambayo inalinda ustawi, kuimarisha mshikamano, kuzuia uchovu wa kupindukia, na kuwawezesha wanaharakati na watendaji kuendelea na kazi kwa muda mrefu ili kuleta mabadiliko ya kijamii.

Kwa hivyo, kampeni ya mwaka wa 2026, itawaleta kwa pamoja wanachama na wadau kupitia majadiliano, utetezi, hatua za kijamii, ushirikishwaji wa vyombo vya habari, na ushirikiano wa kikanda. Jitihada hizi zitaongeza sauti za kuzuia, kuimarisha mshikamano, na kutetea kuhusu upatikanaji wa rasilimali na kuwezesha mazingira yanayohitajika ili kujenga vuguvugu la uanaharakati lililo imara na thabiti zaidi katika kuzuia ukatili.

Mfano wa Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Kuna njia nyingi za kuhusisha vyombo vya habari vya uchapishaji. Badilisha taarifa kwaajili ya vyombo vya habari hapo chini kulingana na muktadha wako na ushirikishe vyombo vya habari vya ndani. Unaweza pia kuwasilisha moja ya picha za Siku 16 zinazowakilisha nguvu ya pamoja na mshikamano wa kifeministi kwenye gazeti au jarida la ndani.

Inaweza kutolewa kwenye vyombo vya Habari moja kwa moja

Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari

Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia mwaka wa 2026

Dhamira: Tengeneza upya mamlaka yetu: Hatua za pamoja kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake

Kauli mbiu: Wezesha. Chukua Hatua. Tengeneza Mustakabali wa Baadae.

Wito wa Kampeni

Wakati dunia ikiadhimisha **Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia**, Mtandao wa Kuzuia UWAKI unatoa wito kwa wanaharakati, jamii, serikali, asasi za kiraia, vuguvugu za kifeministi, wafadhili, vyombo vya habari, na washirika kutengeneza upya mamlaka ya pamoja ili kulinda nafasi ya kiraia, na kuwekeza katika kuchukua hatua endelevu za kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

Kampeni ya mwaka wa 2026 imekuja katika kipindi ambapo masharti muhimu ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake yanazidi kuwa katika shinikizo kubwa. Kote katika kanda, wanaharakati na watendaji wanapitia hali ya kuminywa kwa nafasi ya kiraia, kutokuwa na utulivu wa kisiasa, unyanyasaji mtandaoni, taarifa potofu, simulizi zenye kupinga haki za binadamu, na kupungua kwa rasilimali. Shinikizo hizi zinatishia nafasi za pamoja, sauti, ushirikiano, na juhudi za pamoja zinazohitajika ili kudumisha kuzuia ukatili na kuendeleza usawa wa kijinsia.

Hata hivyo, katika jamii, mashirika ya haki za wanawake, vuguvugu za kifeministi, na juhudi za kijamii zinaendelea kuonyesha ustahimilivu, ubunifu, uongozi, na mshikamano. Jitihada hizo zinatukumbusha kwamba kuzuia ukatili dhidi ya wanawake si jukumu, bali kuchukua hatua endelevu ya kubadilisha mahusiano yasiyo na usawa wa mamlaka, kanuni potofu zitokanazo na mila, na mifumo inayoendeleza ukatili.

Kupitia kampeni ya mwaka wa 2026, Mtandao wa Kuzuia UWAKI unatoa wito wa kuchukua hatua za pamoja zitakazo endelea hata baada ya Siku 16 za Uanaharakati. Serikali lazima ziimarishe hatua wanazopaswa kuchukua ili kuzuia ukatili dhidi ya wanawake kupitia sera, utekelezaji, na ufadhili ulio endelevu. Wafadhili lazima watoe rasilimali zinazonyumbulika na za muda mrefu zinazowezesha mashirika ya kutetea haki za wanawake na vuguvugu za kifeministi. Asasi za kiraia, jamii, na washirika lazima waimarishe ushirikiano, wapinge kanuni potofu zitokanazo na mila, waimarishe ufeministi na sauti zinazoongozwa na jamii, na kusimama kwa pamoja kupinga juhudi zinazodhoofisha haki za wanawake. Nguvu hii ya pamoja lazima iimarishwe, si tu katika kipindi cha Siku 16, bali katika mwaka mzima.

MWISHO

#RenewOurPower | #EmpowerActShapeTheFuture | #16DaysOfActivism